HATI #2 YA UKWELI KUHUSU COVID-19

Taarifa kwa Wateja

Sasisho Lililotolewa: 17 Machi 2020
Imeidhinishwa na Jo Toohey Afisa Mkuu Mtendaji

Hati hii ya ukweli ni ya Wateja wa The Benevolent Society - haifai kusambazwa kwa wengine.

Lengo la hati hii ya ukweli ni kutoa ushauri kwa Wateja kuhusu ushughulikiaji wa The Benevolent Society wa athari za virusi vya Corona (COVID-19).

Virusi vya corona na COVID-19 ni nini?

Virusi vya corona vinaweza kuwafanya wanadamu na wanyama kuwa wagonjwa. Baadhi ya virusi vya corona vinaweza kusababisha ugonjwa unaofanana na mafua ya kawaida na vingine vinaweza kusababisha magonjwa hatari zaidi, ikiwemo Ugonjwa Hatari Zaidi wa Kupumua (Severe Acute Respiratory Syndrome, SARS) na Ugonjwa wa Kupumua wa Mashariki ya Kati (Middle East Respiratory Syndrome, MERS).

Virusi hivi vipya vya corona vilitokea kule Mkoa wa Hubei, Uchina na mkurupuko wa ugonjwa huo unaitwa COVID-19.

Virusi vya corona husambaa vipi?

Virusi vya corona vina uwezekano mkubwa zaidi wa kusambaa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kupitia:

- Mgusano wa moja kwa moja wa karibu na mtu wakati ambapo anaweza kuambukizana (ikiwemo kabla ya kuanza kuonyesha dalili)
- Mgusano wa karibu na mtu ambaye amethibitishwa kuwa ana maambukizi ambaye anakohoa au anapiga chafya; au
- Kugusa vifaa au sehemu (kama vile vishikio vya milango au meza) ambazo zimechafuliwa kutokana na kukohoa au kupiga chafya kwa mtu ambaye amethibitishwa kuwa na maambukizi na kisha kugusa mdomo au uso wako.

Maambukizi mengi husambazwa tu na watu wakati wana dalili. Dalili hizi zinaweza kujumuisha homa, kukohoa, kuwashwa na koo, uchovu na kuishiwa na pumzi. Maambukizi yanaweza pia

kusambazwa kabla ya mtu kuonyesha dalili, kwa hivyo ni muhimu kuzingatia udhibiti mzuri wa maambukizi na usafi kwa ujumla.

Kitaifa, ni hatua gani zinachukuliwa ili kusitisha kusambaa kwa ugonjwa?

Mnamno tarehe 27 Februari, Waziri Mkuu aliwezesha Mpango wa Ushughulikiaji wa Dharura ya Sekta ya Afya ya Australia kwa Ajili ya Virusi Vipya vya Corona (Australian Health Sector Emergency Response Plan for Novel Coronavirus (COVID-19)), ambao ulianzaisha hatua za ziada za kupunguza kasi ya kuingia kwa virusi nchini Australia, na pia kuhakikisha utayari wa kitaifa kwa ajili ya uwezekano wa janga la kiafya la kimataifa. Ushauri unaotolewa kwenye hati hii ya ukweli uanzingatia taarifa iliyotolewa na mamlaka za afya za Serikali Kuu na za Jimbo.

Ushauri wa kina zaidi kuhusu hatua za kujikinga unapatikana kwenye tovuti ya Shirika la Afya Ulinwenguni (World Health Organisation).

Ikiwa utagunduliwa au unashuku kuwa huenda ukawa umeambukizwa COVID-19 – arifu mfanyakazi wa The Benevolent Society mara moja. Tutashirikiana na wewe ili kupata njia mwafaka zaidi ya kukupa huduma. Tafadhali kumbuka kuwa huduma huenda zikasitishwa kwa muda ikiwa wewe ua jamaa wako amegunduliwa kuwa mgonjwa au amelazwa hospitalini.

Ikiwa wewe, jamaa yeyeote au marafiki, wametambuliwa kuwa waligusana na mtu aliyethibitshwa kuwa na maambukizi ya COVID-19, kitengo cha afya ya umma kilicho karibu nawe kitawasiliana nawe kukupa ushauri. Wewe, au jamaa wako, mnahitajika kujitenga kwa kukaa nyumbani kwa siku 14 baada ya kugusana na mtu aliyeambukizwa, na kufuatilia afya yenu na kuripiti dalili zozote.

Kusambaa kwa virusi vya corona kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa ujumla hutokea kati ya watu ambao wanatangamana kwa karibu sana. Mtu unayetangamana naye kwa karibu ni yule ambaye mmekutana uso kwa uso kwa angalau dakika 15, au mmekuwa kwenye nafasi moja iliyofungwa kwa angalau saa 2, na mtu ambaye alikuwa anaweza kuambukizana.

Kitengo cha afya ya umma kitawasiliana na watu ambao wametangamana kwa karibu na wagonjwa wenye maambukizi ya COVID-19. Dalili zozote zikitokea, watu waliotangamana na mgonjwa ni lazima wapigie simu kitengo cha afya ya umma ili kuripoti dalili hizo.

Je, ninahitaji kujitenga ikiwa nimerudi kutoka safari ya ng'ambo?

The Benevolent Society inafuata ushauri wa Idara ya Afya ya Australia (Australian Department of Health) na mamlaka za afya za Jimbo. Kuambatana na ushauri huu, tunatekeleza hatua za kudhibiti zinazohusiana na watu ambao wametembelea maeneo yenye hatari ya juu, au wale ambao huenda walitangamana na virusi.

Ikiwa umesafiri kwenda ng'ambo na umerudi Australia, ni lazima ujitenge kwa siku 14. Kujitenga nyumbani kunamaanisha:

- Usiende kwenye maeneo ya umma kama vile kazi, shule, vituo vya kununua, utunzaji wa watoto

au chuo kikuu
- Muombe mtu mwingine akuletee chakula na vifaa vingine unavyohitaji na aviweke kwenye mlango wako wa nje.
- Usiwaruhusu wageni kuingia ndani – ni watu unaoishi nao pekee ndio wanapaswa kuwa nyumbani kwako
- Hakikisha unakaa kwenye chumba kimoja nyumbani ili usiwaambukize jamaa wale wengine. Taarifa zaidi kutoka health.gov.au

Sajili kuu ya wateja ambao wanahitajika kujitenga nyumbani itawekwa kwenye Ofisi ya Kitaifa ya Benevolent Society, na inaweza kufikiwa na Timu ya Kudhibiti Janga ya Benevolent Society na wafanyakazi wengine wakuu. Sajili hiyo itajumuisha taarifa zifuatazo:

- Jina la mteja
- Huduma iliyotolewa
- Mwasiliani mkuu katika The Benevolent Society
- Tarehe ya kuanzia na sababu ya kujitenga
- Tarehe anayotarajiwa kurudi kazini.

Ni nani mwingine anahitaji kujitenga?

Wateja ambao wametangamana kwa karibu na **mgonjwa aliyethibitishwa** kuwa na virusi vya corona ndani ya siku 14 (lazima ajitenge kwa siku 14 baada ya tarehe ya siku ya mwisho ya kutangamana na mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na virusi hivyo).

Tafadhali zungumza na mwasiliani wako katika The Benevolent Society ikiwa una wasiwasi au maswali yoyote kuhusu hati hii ya ukweli.

Piga simu kwa **1800 236 762** au utume barua pepe kwa: customercare@benevolent.org.au